# Mkutano wa Mawakili wa Serikali 2022

## Mafanikio na Changamoto Kutokana na Maboresho Yanayoendelea Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

**Oswald H.Tibabyekomya**

**Mkurugenzi-NPS**

# Utangulizi

- OTM ilianzishwa tarehe 13 Februari, 2018 kufuatia mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 48/2018 & 49/2018 la tarehe 13 Februari 2018.
- Kabla ya hapo OTM ilikuwa Idara katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo ilikuwa imepangiwa Mawakili 364 na Katibu Sheria 56 ili kuiwezesha ili kuiwezesha kutekeleleza majukumu yake ya kusimamia na kuendesha na kuendesha mashtaka ya jianai.
- Malengo mahususi ya uanzishwaji wa OTM ni kuimarisha na kuongeza uwezo wa uendeshaji wa mashauri ya jinai, kuongeza ufanisi wa utenganishaji wa shughuli za upelelezi na mashtaka na kuimarisha na kuongeza usimamizi na uratibu wa uendeshaji wa

# Muundo

- Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka akisaidiwa na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka kama Msaidizi Mkuu wa Mkurugenzi wa Mashtaka.
- Aidha, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Afisa Masuuli na Mamlaka ya nidhamu.
- Ofisi ina Divisheni Sita (**6**), Vitengo Saba (**7**), Sehemu Kumi na Nane (**18**) na Ofisi za Mikoa Ishirini 26 na Ofisi Maalum za Mikoa ya Kimashtaka 4 na hivyo kufanya Ofisi za Mikoa kuwa (**30**) ya kimashtaka na Ofisi za Wilaya Kumi na Nne (**14**).

# Majukumu

- Majukumu yameainishwa katika Hati Idhini ya Uanzishwaji wa OTM, Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka na Sheria nyinginezo.
- Majukumu hayo ni pamoja na:

✓ Kuamua kufungua au kutofungua mashtaka;

✓ Kusimamia na kuendesha kesi zote za jinai kwa niaba ya Jamuhuri;

✓ Kuratibu na kusimamia upelelezi wa makosa ya jinai;

✓ Kuendesha au kutetea rufaa zinazokatwa dhidi ya Jamhuri

✓ Kuwasimamia Mawakili wa Serikali na Waendesha Mashtaka; na

✓ Kusimamia ufifilishaji wa makosa ya jinai unaofanywa na taasisi nyingine;

# Utekelezaji wa Majukumu

- **Uratibu wa shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai**

✓ OTM imetoa miongozo mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha uratibu upelelezi wa makosa ya jinai ikiwemo Mwongozo wa Kufungua Mashtaka, 2022; Taratibu za Utendaji Kazi katika Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka yanayohusu makosa ya Rushwa, makosa dhidi ya watoto na usafirishaji haramu wa binadamu

✓ Kufanya kazi na wapelelezi katika hatua za awali za upelelezi, Kupitia majalada ya upelelezi ya muda mrefu na kutembelea magereza na sehemu walikohifadhiwa mahabusi.

✓ Matokeo ya hatua hizi, kesi zinafunguliwa upelelezi ukiwa umekamilika isipokuwa kwa makosa ambayo yameruhusiwa na sheria, hakuna malalamiko ya kuchelewesha upelelezi kesi za mauaji, uhujumu uchumi na utakatishaji fedha.

# Utekelezaji Majukumu…

- **Usimamizi na uendeshaji wa mashtaka**

✓ Umeimarishwa kwa

❖ kutoa Mwongozo wa Kufungua Mashtaka, 2022; Taratibu za Utendaji Kazi katika Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka yanayohusu makosa ya Rushwa, makosa dhidi ya watoto na usafirishaji haramu wa binadamu;

❖ Kuimarisha usimamizi wa shughuli za mashtaka kwa kufanya tathmini kila mwezi na kaguzi za mara kwa mara

✓ Kutokana na hatua hizi zilizochukuliwa kasi ya kusikiliza na kukamilisha kesi imeongezeka. Kwa mfano katika kipindi cha Julai 2021 hadi Julai 2022 uendeshaji wa kesi ni kama ifuatavyo:

# Utekelezaji wa Majukumu…

- Katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi, jumla ya kesi **48,720** ziliendeshwa, kesi **32,650** sawa na 67% zilihitimishwa kesi **16,070** sawa na 33% zinaendelea ktk hatua mbalimbali.
- Mahakama za watoto, jumla ya kesi **920** ziliendeshwa, kesi **677** sawa na 74% zilihitimishwa, kesi **243** sawa na 36% zinaendele ktk hatua mbalimbali
- Mahakama Kuu, jumla ya kesi **6,035** zilifunguliwa, kesi **1,299** zilipangiwa vikao na kukamilika kwa 100%, kesi **4,736** zinasubiri vikao.

# Utekezaji wa Majukumu…

- **Urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu**

✓ Katika kipindi cha miaka 4, OTM imeendesha kesi mbali mbali ambazo zimehitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani kuamriwa kurejesha mali na pia kufungua maombi 53 ya kurejesha kurejesha mali mali zinazohusiana na uhalifu

✓ Mali zilizorejeshwa ni pamoja na:

❖ Fedha jumla ya Sh. **17,269,303,396.97** na USD **9,210,218.36;**

❖ Madini mbambali yenye thamani ya Sh. **101,483,106,126.05** yalitaifishwa;

❖ Mbao **6,304** na magogo 18,409 ya mti aina ya African Rosewood.

❖ Nyumba arobaini na tatu (4**3),** Mashamba 6 na Viwanja 7; na

❖ Magari 184 na Piki Piki 119;

# Utekelezaji wa Majukumu…

- **Ushughulikiaji kesi kwa utaratibu wa watuhumiwa kukiri kwa hiari**

✓ Kuanzia mwaka 2019 OTM imeanza kushughulikia kesi kwa utaratibu wa maridhiano ya kukiri kosa la jinai

✓ Kesi nyingi zimeshughulikiwa na kupunguza mrundikano wa kesi

✓ Fedha zinazohusiana na hualifu pia zimerejeshwa. Hadi kufikia Agosti 2022 jumla ya kiasi cha Shilingi 53,000,000,000 zilirejeshwa kutokana na kesi zilizohitimishwa kwa utaratibu wa plea bargaining.

✓ Fedha hizi zinajumuisha fidia kwa wathirika wa matukio ya uhalifu ambao ni Serikali na waathirika binafsi na faini walizolipa kama sehemu ya adhabu ya makosa waliyokiri.

# Utekelezaji wa Majukumu…

- **Utenganishaji wa shughuli za mashtaka na upelelezi**
- ✓ Ofisi za mikoa zimefunguliwa katika mikoa yote 26 na mikoa mingine 4 maalum ya ya kimashtaka.
- ✓ Ofisi za Wilaya 18 kati ya Wilaya 139.
- ✓ Kesi nyingi za jinai katika mahakama za Wilaya bado zinaendeshwa na Waendesha Mashtaka kutoka katika vyombo chunguzi.
- ✓ Wapo waendesha mashtaka 779 ambao wanasaidia kuendesha kkesi katika mahakama za wilaya.

# Utekelezaji wa Majukumu…

- **Maendeleo ya Rasilimali watu**

✓ OTM imeendelea kuchukua hatua kuongeza raslimali watu.

❖ Mfano mwaka 2018 wakati inaanzishwa ilikuwa na Mawakili 364 na Katibu Sheria 56, hadi kufikia Juni, 2022 ilikuwa na jumla ya watumishi 613 na kati ya hao Mawakili wa Serikali ni 425

❖ Hivi karibuni OTM inatarajia kuajiri Mawakili wa Serikali 82 na na Makatibu Sheria 20.

✓ Ofisi inaendelea kujenga hoja ya kuongezewa watumishi

# Utekelezaji wa Majukumu…

- Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.
  - ✓ OTM imeanza utekelezaji wa mradi wa majengo ya Ofisi ambapo majengo matano ikiwemo moja (1) la makao Makuu Dodoma, 1 katika Mkoa maalum wa kimashtaka Ilala, 3 katika Mkoa wa Pwani, Morogoro na Mbeya na inashirikiana na OAG kujenga Ofisi Jumuishi ya Mkoa wa Mwanza.
  - ✓ Ujenzi wa Ofisi pia umeanza katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Njombe, Manyara, Shinyanga na Geita.
  - ✓ Ofisi hizi zikikamilika zitasaidia siyo tu Mawakili wa Serikali waliopo NPS bali pia Mawakili wa Serikali waliopo OAG na SG waliopo katika maeneo hayo

# Mafanikio

- Kuimarika kwa ushirikiano na wadau
- ❖ Vyombo chunguzi na taasisi nyingine
- Kupungua kwa msongamano wa mahabusu magerezani
- Kupungua kwa mrundikano wa kesi mahakamani
- Kurejesha fedha kutoka kwa wahalifu na kupunguza faida katika uhalifu

# Changamoto

- **Upungufu Mkubwa wa Rasilimali**

✓ Watumishi waliopo kwa sasa

✓ Mahitaji halisi

- **Upungufu Mkubwa wa Rasilimali fedha**

✓ Kibajeti Ofisi imekuwa ikipewa Ukomo Mdogo wa Bajeti ikilinganishwa na aina na ukubwa wa majukumu ya Usimamizi na Uratibu iliyonayo.

- **Kutokuwa na Majengo ya Ofisi.**

✓ OTM haina majengo ya  katika ngazi zote kuanzia Makao Makuu, Mikoa na Wilaya ispokuwa katika mkoa wa Iringa na Ofisi ya Mashtaka ya Wilaya Serengeti.

# Changamoto…

- **Uhaba wa magari na vitendea kazi.**
  Ofisi za Mikoa na Wilaya bado zinakabiliwa na uhaba wa vitendea kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kiofisi licha ya hatua mbali mbali zilizochukuliwa;
- **Kutokuwa na Motisha na mazingira hatarishi ya kazi**
  Kutokuwepo motisha wa kipekee kwa watumishi kutokana na mazingira magumu na hatarishi ya utendaji kazi.
- **Kutokuwepo Kwa Bajeti Maalumu kwa ajili ya Programu ya Kutenganisha Kazi za Upelelezi na Mashtaka.**
  Hii ni programu kubwa inayohitaji fedha za ziada. Kwasasa utekelezaji wake hutegemea zaidi fedha kutokana na bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ambazo hazitoshelezi.

# Changamoto…

- Kutokuwasilishwa kwa taarifa za ufifilishaji wa makosa jinai yanayofanywa na taasisi nyingine za Serikali;
- Ushiriki mdogo wa wanasheria katika kuzuia ukiukwaji wa sheria zinazotengeza makosa ya jinai

✓ Sheria ya Manunuzi ya Umma

- Makosa mengi yanatokana na ukiukwaji wa sheria ya manunuzi
- Makosa haya yanaweza kupungua kama Mawakili wa serikali watashauri vizuri

- Uzingatiwaji mdogo wa sheria zinazotengeza makosa ya jinai yanayosimamiwa na taasisi zisizochunguzi.

-Workers Compensation Act

-Waajiri hasa katika Halmashauri hawasilishi michango ya watumishi.

# Mikakati ya Kutatua Changamoto

- OTM inaendelea kuchukua hatua na kujenga hoja Serikalini ili:
  - ✓ Kuongezwa kwa bajeti ili kukabiliana na changamoto nyingi zinazotokana na ukomo wa bajeti;
  - ✓ Kupewa vibali vya ajira kwa ajili ya kuongeza idadi ya Mawakili na Watumishi wengine;
  - ✓ Kuwepo na programu maalumu kwa ajili yakufanikisha kutenganisha shughuli za Upelelezi na Mashtaka;
  - ✓ Kuboresha motisha na mazingira ya kazi kwa watumishi;
  - ✓ Kuwepo na program maalumu ya kuongeza rasilimali watu; na
  - ✓ Kuhakikisha inapata majengo ya Ofisi katika Mikoa na Wilaya zote.
- Kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau

# Hitimisho

- Katika kipindi cha miaka 4 tangu kuanzishwa kwake OTM imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia na kuendesha mashtaka ya jinai licha ya changamoto zilizojitokeza.

- Ofisi inaendelea kuchukua hatua kutatua changmoto zilizopo na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha inatimiza dira yake ambayo ni **‘Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa.**